

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA  
(TAMISEMI)

MTIHANI WA UTIMILIFU KANDA YA KUSINI  
(MIKO YA LINDI NA MTWARA)

121/2

KISWAHILI 2

(Kwa watahiniwa walioko na wasiokuwa shulenii)

Muda: Saa 3

2024

---

**Maelekezo kwa Watahiniwa**

1. Mtihani huu una sehemu A na B zenyenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote sehemu A na sehemu B jibu maswali **matatu (3)** swali la **sita (6)** ni la lazima.
3. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
4. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

**DYAMPAYE.CO.TZ**

Mtihani huu una kurasa tatu zenyenye maandishi

## SEHEMU A (ALAMA 40)

Jibu maswali **yote** kutoka sehemu hii.

1. Ili kazi ya fasihi ikamilike inahitaji uwepo wa wahusika ambao ndio watendaji wakuu. Tumia kigezo cha tabia ya wahusika kueleza aina kuu nne (4) za wahusika wa fasihi.
2. Moja ya Riwaya zilizojipatia umaarufu mwishoni mwa miaka ya tisini nchini Tanzania ni Riwaya pendwa ya salamu kutoka kuzimu yenyenye mhusika Joram Kianga. Onesha sifa bainifu tano (5) za Riwaya pendwa.
3. “Fasili andishi haiwezi kufanana na fasihi simulizi”. Thibitisha kwa hoja tano (5) zenye kuonesha sifa bainifu za fasihi andishi.
4. Soma shairi lifuatalo, kisha eleza mbinu za kifani zilizotumika

## TANGAZO TANGAZO

1. Tangazo! Tangazo! Meli karibu kuzama!  
Kila asikiaye tangazo ajiweke tayari, kuiokoa nafsi,  
Nchi kavu imekuwa finyu, maji yameivamia  
Hakuna pa kukimbilia
2. Enyi wakulima jihadharini,  
Mihogo shambani imekwisha,  
Ngurue wamestuka,  
Kazi hufanya usiku na mchana,  
Sasa tufanye nini?  
Njaa yasimama mlangoni, hodi yabisha ajabu.

## SEHEMU B (ALAMA 60)

Jibu maswali **matatu** (3) kutoka sehemu hii swali la **sita** (6) ni la lazima.

## ORODHA YA VITABU

### (A) USHAIRI

Kimbunga	-	Haji G. Haji
Mapenzi Bora	-	Shaban Robert
Chungu tamu	-	Theobald Mvungi
Fungate ya Uhuru	-	Mohamed S. Khatibu

### (B) RIWAYA

Usiku utakapokwisha	-	Mbunda Msokile
Kufikirika	-	Shaban Robert
Mfadhili	-	Hussein Tuwa
Vuta N'kuvute	-	Shafi Adam Shafi

**(C) TAMTHILIYA**

Kwenye Ukingo wa Thim	-	Ibrahim Hussein
Morani	-	Emmanuel Mbogo
Kivuli kinaishi	-	Said Mohamed
Nguzo Mama	-	Penina Muhando

5. “Waandishi wa ushairi ni askari ambao hawalali wala hawasinzii, daima wapo macho kuzilinda jamii zao dhidi ya mambo mbalimbali”. Thibitisha kauli hii ukirejelea diwani mbili ulizosoma darasani kwa hoja nne (4) kwa kila diwani.
6. Ugomvi kati ya washairi wa kale na washairi wa usasa upo kwenye muundo. Kwa kutumia diwani mbili (2) ulizosoma eleza vipengele vinne (4) vijengavyo shairi la kimapokeo.
7. “Mwaka 1995 kulikuwa kilele cha mwanamke duniani kupitia mkuu wa wanawake uliofanyika Beijing nchini China”. Tumia tamthiliya mbili (2) ulizosoma kuonesha nafasi ya mwanamke katika jamii kwa hoja nane (8).
8. “Waandishi wa riwaya toka zamani wamekuwa wakijadili kwa kinagaubaga dhana ya huruma ndani ya jamii”. Thibitisha usemi huu ukutumia riwaya mbili (2) ulizosoma darasani kwa hoja nane (8)